# Nafasi ya Wahusika Jumui katika Ujenzi wa Maudhui: Mifano kutoka Riwaya za Kimajaribio za Kiswahili

*Joyce A. Obetch, James O. Ontieri* na *Mark A. Odawo*
*Chuo Kikuu cha Rongo*

**Ikisiri**

**Utunzi wa kazi za sanaa huhitaji ustadi mkubwa katika uteuzi na usawiri wa wahusika. Kutokana na umuhimu wao katika kazi yoyote ile ya fasihi, wahusika husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kufanikisha ujenzi wa maudhui na vilevile kuwakilisha dhana mbalimbali zinazoakisi maisha katika jamii (Msokile, 1992). Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu usawiri wa wahusika jumui katika riwaya za Kiswahili za kimajaribio lakini kwa uelewa wetu, nafasi ya wahusika jumui katika ujenzi wa maudhui haijashughulikiwa kikamilifu. Kwa mujibu wa hoja hii, makala haya yanajadili jinsi usawiri wa wahusika jumui katika riwaya teule za kimajaribio za *Babu Alipofufuka* (2001) na *Dunia Yao* (2006) unavyowasilisha maudhui ya kihalisia. Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi kutokana na uwezo wake wa kutoa data yakini zilizotosheleza mahitaji ya utafiti huu. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini wa riwaya teule, kisha zikachanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kinathari. Utafiti ulionesha kuwa wahusika jumui wametumiwa kujenga maudhui ya utandawazi, utamaduni mpya, utabaka, uongozi mbaya na sanaa mpya katika riwaya teule. Matokeo haya yataongeza maarifa ya uhakiki wa kitaaluma wa kazi za fasihi na utunzi wa kiubunifu.**

**Maneno Muhimu:** *Maudhui, Riwaya za Kimajaribio, Wahusika Jumui*

## Utangulizi

Kwa mujibu wa Bergonzi (1972), awali uhalisia katika kazi za fasihi ulikuwa njia bora ya kuwasilisha maudhui. Hii ni kwa sababu ya uwazi na mtiririko wake wa kimantiki. Bergonzi anasema kuwa hii ilikuwa njia bora ya kufichua na kuelezea umma matatizo ya kijamii na kisiasa. Pia, uhalisia huu ulikuwa muhimu katika kuelewa historia ya riwaya hizo. Wataalam wengine kama vile Walibora (2010) na Khamis (2010) wanakubaliana kuwa riwaya tangulizi zilijikita katika uhalisia mkavu. Kwao, Riwaya ya Kimajaribio ni utanzu wa fasihi uliopata uamuzi wa mabadiliko ili kuepuka kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji. Mabadiliko haya ni kuondoka kwa kazi ya fasihi kutoka sura iliyozoeleka na kwenda sura mpya. Upya huu umo kwenye usanii na maudhui. Majaribio yenyewe hulenga katika kukiuka kaida zilizozoeleka za kiutunzi wa riwaya na kutokeza mtindo mpya usiofanana na ule wa kijadi. Sifa kubwa ya riwaya za namna hii huonekana katika mchanganyiko wa matukio, matumizi ya fantasia na mazingaombwe, mwingilianomatini, uchanganyaji wa historia na ubunifu, matumizi ya wahusika jumui na wa kidhahania na mandhari dhanaishi. Kwa mujibu wa Lee (2004), mhusika jumui ni yule anayeundwa na watu wawili au zaidi wa maisha halisi, watu wa kubuni au wasio wa kubuni.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisiamazingaombwe. Hii ni nadharia ya fasihi ambayo kwayo mipaka kati ya uhalisia na udhahania umefutwa na huchanganya masuala ya kihalisia na yale ya kiajabuajabu. Mambo yanayumbishwayumbishwa baina ya ulimwengu wa kihalisia, wa kufikirika na wa kimiujizamiujiza. Kwa mujibu wa Zamora (1995), nadharia ya Uhalisiamazingaombwe iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani Franz Roh. Roh anasema kuwa, Uhalisiamazingaombwe ni uwasilishi wa ujumbe unaofichua hali ya kiroho na umazingaombwe katika chombo kwa kubainisha kudhihirika kwake na kuifanya kuwa halisi. Chanady (1985) anasema kuwa uhalisiamazingaombwe unahusu matukio yasiyo ya kawaida au ya miujiza au chochote kilicho kinyume na uhalisia wa kawaida. Mhimili wa 'wahusika wa kawaida, wenye nguvu za kiajabu au wasio wa kawaida/kihalisia kama vile mazimwi, mashetani, wafu, vizuu, mizuka na kadhalika hutumiwa kusawiri maudhui ya kihalisia' ulitumiwa kuchanganua maudhui katika riwaya teule. Watafiti waliongozwa na taratibu za mhimili huu zilizohusisha kutambua maudhui mbalimbali yanayowasilishwa na jinsi ambavyo wahusika jumui wametumiwa kuyakuza. Pili, walifasiri athari za maudhui hayo kwa jamii.

Utafiti huu ulitumia mbinu ya upekuzi kwa kusoma kwa makini, kutalii na kuchunguza riwaya teule zenye maumbo ya kimajaribio maktabani. Utafiti huu aidha ulipekua maandishi ya awali yanayoelezea sababu za kuzuka kwa wahusika jumui katika fasihi pamoja na machapisho, tasnifu na tafiti nyingine zinazoshughulikia dhana ya fasihi ya majaribio. Maandishi hayo yalikuwa amilifu katika uchanganuzi wa maudhui yaliyowasilishwa na wahusika jumui katika riwaya za *Dunia Yao* na *Babu Alipofufuka* kisha data zikawasilishwa kinathari. Riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi kutokana na uwezo wake wa kutoa data yakini zilizotosheleza mahitaji ya utafiti huu.

**Matokeo ya Utafiti**

Kwa mujibu wa utafiti huu, wahusika jumui waliotumiwa na mwandishi wa riwaya za kimajaribio kujenga maudhui mbalimbali ni Ndi katika *Dunia Yao* na K katika *Babu Alipofufuka.* Maudhui hayo ni kama ifuatavyo:

***Utandawazi***

Friedman (2005) anasema kuwa utandawazi ni neno lililoanza kutumika miaka ya 1990, likimaanisha kukifanya kitu kuwa katika kiwango cha kimataifa na kukihamisha nje ya mipaka, kukiweka wazi kikafanywa na watu wa aina yote duniani. Alomo (2016) anaeleza utandawazi kama mahusiano ya kimataifa ya binadamu na taasisi mbalimbali yanayorahisishwa na teknolojia ya mawasiliano. Jerono (2016) naye anaafiki mawazo haya anapoeleza utandawazi kama mchakato unaofanikishwa zaidi kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano kuunganisha jumuia ya dunia kuwa mfumo mmoja wa kiuchumi na kijamii. Kimsingi, utandawazi unasisitiza uondoaji wa vikwazo vya kibiashara na kuifanya dunia kuwa soko moja. Unahimiza soko huria, demokrasia, utawala bora, usawa wa kijinsia na haki za binadamu (Murithi, 2017).

Katika riwaya ya *Dunia Yao,* Bi Muse, malkia wa sanaa, ambaye si kiumbe wa kihalisia anamwingia Ndi kichwani na kumweleza umuhimu wa kutumia teknolojia katika kuandika simulizi zake. Mhimili wa 'wahusika wa kawaida, wenye nguvu za kiajabu au wasio wa kawaida kama vile mazimwi, mashetani, wafu, vizuu na mizuka hutumiwa kusawiri maudhui ya kihalisia' ulitusaidia kuchanganua maudhui haya. Ndi hakuelewa kama alikuwa ndotoni au la lakini alijikuta ameshazama ndani ya maneno yake. Aliamua kutumia kompyuta katika kuandika simulizi zake kwa wasomaji wake badala ya kutumia mdomo. Anasema:

> Labda ingetosha simulizi ya mdomo baada ya weusi na weupe. Aaaa niliamua, kwa maslahi ya wasomaji, hatimaye niwasilishe kadhia hii kisimulizi maandishi (uk. 61).

Kupitia kwa dondoo hili, mwandishi anasisitiza umuhimu wa kutumia kompyuta katika uandishi wa kazi ya fasihi kwa sababu kazi hizo sasa zinaweza kuwafikia wasomaji wengi mno ikilinganishwa na fasihi ya mdomo. Pia, fasihi yenyewe haibadilishwibadilishwi toka kwa msimulizi mmoja hadi mwingine. Kila msomaji anapata ujumbe uliokusudiwa tangu mwanzo na mwandishi wa kazi husika. Khamis (2010) anamnukuu Kettle (1959) ambaye anatetea katika uandishi wa riwaya kuwa, mapinduzi makubwa katika jamii za watu hubadilisha urazini na si kupindua hisia zao za kijamii tu bali pia mitazamo, falsafa na sanaa zao.

Ndi akimsimulia Bisudi hadithi yake, katika uhalisiamazingaombwe, anaruka juu katika maono na kushuhudia jinsi dunia yao ilivyo na machafuko. Ndi anasema kuwa alijikuta anavutwa, kuruka na kuleja hewani kama kwembe juu ya Bahari ya Hindi na huko akatuwama kutazama upeo wa macho kwenye dunia yao. Mwandishi anasema kuwa alipotazama, aliona pande mbili tofauti na kuona utofauti mkubwa uliopo. Anasema:

> Magharibi ya kaskazini, niliwashuhudia watu waliojipweteka juu ya morischea wanakula raha za maendeleo yaliyotekenywa zaidi na teknolojia, hasa ile ya 'high-tech' na mawasiliano ya 'digital'; tabasamu ya kwishafika inawaenda midomoni mwao. Lakini kusini na mashariki niliona watu wakitimika timtim mbio hemkahemka, wacheza ngoma tu… na hofu, na kukata tamaa, wasiwasi, woga na mchukuo wa kinyama… Huyu kakamata rungu. Mwingine ana panga. Yule kashika kigongo na mwenzake kainua mrau. Maneno.

> Kutukanana, kusimbuana, kulana roho. Kuangamizana. Mradi ugomvi. Fujo na vita vya wenyewe kwa wenyewe visivyokwisha (uk. 212).

Mwandishi, kupitia maelezo hayo ya Ndi alipokuwa njozini, anaeleza juu ya maendeleo yanayoletwa na teknolojia. Anaonesha jinsi ambavyo nchi zilizoikumbatia teknolojia zinavyoendelea na zilizoikataa zinavyosalia katika umasikini na vita vya mara kwa mara. Ruigrokna Tulder (1995) amesifia mchakato wa utandawazi hasa katika nchi zinazoendelea. Anasema kuwa hatimaye utaboresha maisha ya watu wote duniani. Pia, anatambua utandawazi kama ngazi ya biashara baina ya nchi, masoko huru ya bidhaa na kutangamanisha tamaduni mbalimbali.

Baadaye, Ndi anarudi uhalisini na anasema kimoyomoyo kuwa mwanya wa mamilioni ya miaka uliyatenga makundi hayo mawili. Mwanya unaashiria matabaka mbalimbali. Kwa mujibu wa Marx (1973) matabaka huwa katika hali ya mikinzano na kwa sababu jamii daima ziko katika harakati za kufanya maslahi yao bora, mikinzano hii huleta mapinduzi na uongozi kuchukuliwa na tabaka la wafanyakazi na mafalahi. Naye Althusser (1981) anasema, tabaka tawala hukazania kupinga na kudhibiti wafanyakazi na wale wanaonyanyaswa kwa njia zozote zile aidha kwa matumizi ya nguvu au vyombo vya kiitikadi.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, K anapofika Neo-casino, watukufu kama vile Di-Livio, Miyawaza, Delpiero na Von Heim walifika langoni kama nyukijeshi kuja kumlaki na kumwonesha hamu yao ya kumbeba. Kupitia kwa maelezo hayo, mwandishi anatujulisha kuwa:

> … habari huenda kwa kompyuta siku hizi. Walikuwa tayari wameshapata habari ya K kuzungukwa na wahuni kule njiani (uk. 29).

Mwandishi anaeleza kuwa kupitia kwa teknolojia, watu huweza kupata habari ya mambo yote yanayofanyika kote duniani kwa wakati. Hivyo anasisitiza umuhimu wa teknolojia pale inapoweza kutumiwa kuokoa maisha ya mwanadamu.

K anaamka kwa mlio wa Doggy uliotoka kwa kompyuta. Kila kitu ndani mwake kilikwenda kwa kompyuta, bafu lilijazwa maji yenye ufufutende wa kiasi na kompyuta. Alikimbilia chumba chake cha kompyuta kubofya kibodi kuamrisha chumba cha mbwa, chumba chake na bwawa lisafishwe haraka (kur. 52-63). K aliusogelea mlango wa msalani na hapohapo mlango ukafunguka. Hapo msalani, flashi lilijipapia maji. Alipoketi tu na flashi ikaavya maji alipoondoka baada ya kumaliza haja yake. Aliwasha swichi na kuanza kupiga mswaki (uk. 65). Kompyuta yamwambia K akiwa chumbani mwake kuwa mkewe Bi Kikuba alikuwa akimsubiri katika kumbi la chini (uk. 67). Kupitia kwa maelezo hayo, mwandishi anamtumia K kutujulisha jinsi ambavyo utandawazi umerahisisha mambo katika maisha ya mwanadamu.

Japo utandawazi umeoneshwa kama wenye faida kwa kiwango fulani, kuna wataalamu ambao wanailaumu kwa kuzorota kwa mila, tamaduni na desturi ya mataifa yanayoendelea. Gromov (1998) anafafanua kuwa waandishi wa Riwaya za Kimajaribio wanaonesha hasira zao kwa kile wanachoona ni ujinga wa viongozi au serikali zetu kukubali kiholela kuhonga nchi kwa mataifa makubwa. Katika *Dunia Yao*, Ndi akiwa ndotoni, mwandishi anatumia joshijitu ili kuonesha hatari na maafa ya utandawazi katika jamii yake. Anaonesha kuwa utandawazi uko kila pahali bila idhini wala hiari ya wanajamii (uk. 189). Alomo (2016) anasema kuwa, riwaya mpya hueleza jinsi kumekuwa na mabadiliko hasi kwa sababu ya utamaduni mpya. Anasema japo inadhihirika kuwa wanajamii hawataki tamaduni mpya, hawawezi kuizuia. Ndi anaona jitukitu ambalo umbo lake limeunganishwa nusu kwa nusu, kushoto na kulia katikati ya jimwili lake. Pandikizi la jitukitu jinsi lilivyoumbika, ulikuwa ukipita kwa kasi ya umeme, lakini lilionekana upo papo hapo daima – haliondoki! Linapiga kasi katika njia yake inayojiandika yenyewe mara *Globalization* mara *Americanization*. Likapita kwa kasi na pepo zake za dhoruba likiripuka mandimi ya moto yaliounguza na kukausha kila kitu: watu, wanyama, barabara, majumba, miji na majiji, mashamba, mazao ya chakula, mazao ya mauzo, miti, maji, hewa, …tamaduni na hata uhai, heshima na mustakabali wa watu – hata roho zao, kisha kuangamiza lilivyopenda (kur. 205-206).

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, kasri la K limejaa watu kama utitiri; walinzi wa siri, walinzi wa dhahiri, makarani, wapishi, wasafishaji, wahudumu bustani, waduhushi-mbwa-na-farasi, madereva, mayaya na madobi. Watu hawa wote hupotelea mbele ya jicho lake mpaka pale anapomhitaji mmoja wao na kufumbua akili ya kompyuta kuweza kumwita na kumtuma haja yake (uk. 16). Hii ni mojawapo ya athari za utandawazi. Mhusika K anatumia mtandao kufanya karibu kila kitu, haoni umuhimu wa kuongea na kushirikiana na watumishi wake katika kasri hili. Kwa njia hiyo, teknolojia inaleta utengano baina ya wanadamu.

***Utamaduni Mpya***

TUKI (2013) inafasiri utamaduni kama mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani. Alomo (2016) anasema kuwa, utangamano au mahusiano baina ya tamaduni mbalimbali umezaa utamaduni mpya ambao hudhihirika kupitia mavazi, vyakula, mila, hadithi na mengine. Kwa mujibu wa Riwaya za Kimajaribio, utamaduni wa nchi zenye nguvu huathiri utamaduni wa nchi zisizo na nguvu na hivyo utamaduni wao hutawala. Utamaduni mpya unaotokana na mataifa yenye uwezo husawiriwa kama donda ndugu katika mataifa changa, haswa wanapoiga kila kitu kutoka kwao bila kupiga msasa. Athari za kuiga kila kitu ni bayana katika Riwaya za Kimajaribio.

Katika *Dunia Yao*, Muse anamtembeza Ndi kwenye bustani zake na kumwonesha tofauti iliyopo kati ya mataifa yaliyoukumbatia utamaduni mpya na yale yaliyokataa kwa ukorofi. Muse katika umazingaombwe anamwambia Ndi:

> Unaona kule jinsi vi-villa vyema vinavyochipuka? Kama uyoga. Vinasimama kwa fahari ya utamaduni mpya. *It's beautiful… fantastic!* Ipeleleze mishahara yao…Na kisha geuka huku. Unaona wingi wa vibanda vya ukorofi vile vilivyojiinamia kwa fedheha, kule ambako wivu na uchungu ulianza na kuendelea enzi na azali (uk. 65).

Mohamed anaeleza jinsi ambavyo mabadiliko yanavyoshuhudiwa katika maeneo ambayo yamekubali kuacha tamaduni zao na kukumbatia utamaduni mpya. Anasema kuwa maisha yao yamestawi kwani mishahara yao ni ya juu. Kwa upande mwingine, wale ambao wamekwamilia tamaduni zao wanaishi katika umaskini na fedheha kuu.

Utandawazi umekwisha ondoa mipaka na kuufanya ulimwengu jiji moja na kuathiri utamaduni kabisa. Kupitia kwa usimulizi wake, Mohamed anaonesha imani kuwa mavazi na mienendo ya Yungi imechangiwa pakubwa na utandawazi anaposema:

> Hii ni fensi mpya, *Carnival* ya *globalization* na kwa hivyo kila mtu alivaa kivyake, alijifanya kinyago kivyake. Hakuna adabu, heshima au kujuliana. Hakuna ubaba au ubinti (uk. 107).

Mwandishi anaonesha kuwa utamaduni umeathirika sana kwa sababu ya utandawazi. Anadhihirisha hili kupitia kwa mavazi ya Yungi yaliyomwonesha uchi. Pia, majibizano baina ya Yungi na babake, ni uzao wa utandawazi ambapo mtoto anaweza kumkosea mzazi heshima na kujibizana naye. Vijana kote duniani, sasa wana utamaduni wao ambao Brake (1980) anaueleza kama 'ulimwengu huru' wenye mitindo na njia za maisha ambazo wao hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao.

Katika *Babu Alipofufuka*, hakuna hakika ya chakula, makazi, elimu, matibabu, …heshima ya uafrika ambao tokea mwanzo ulikuwa umekandamizwa sana wakati wa ukoloni. Mzuka anashangaa kuona K anapokula chatu wa kutokosa, nyoka wa kukaushwa, kijibwa kilichochomwa, nyama ya nyangumi aliyekaangwa na kukatwakatwa vipandevipande. Hili lamshtua Mzuka kwani vyakula hivyo vingekuwa asili ya Kiafrika, bila shaka ingekuwa hadithi ya kima na tumbili wa Zaire. Isitoshe, vyakula ambavyo vilijulikana kama vya kimsingi vimewekewa dawa kwa lengo la kuzidisha uzalishaji. Dawa hunyunyiziwa mimea hii na hata kuwekewa rutuba za kunawirisha afya yao. Kemikali katika mimea hii kutokana na dawa inayonyunyiziwa na rutuba imekatisha afya ya walaji. Aidha, vyakula vinavyotokana na mifugo vimekuwa tishio kwa afya ya binadamu.

Katika *Dunia Yao*, kupitia kwa mazungumzo baina ya Ndi na Shaib, mhusika wa kimazingaombwe, ni bayana jinsi utamaduni mpya ulivyoathiri afya ya wananchi. Ndi anamweleza

Shaib kwamba miili ya watu ilijazwa sumu kupitia nyama ya ng'ombe, kuku, kondoo, nafaka na mboga. Hizo zilidhihirika katika dawa za kunyunyizia mimea na dawa za mifugo (uk. 49).

Pia, mwingiliano wa tamaduni mbalimbali umeweza kuzorotesha mila za nchi. Kwa mfano, ijapokuwa FKK ni klabu kama yoyote ile ambako watu huenda kustarehe, wote watakaoingia kule watakuwa uchi. Mila za Kiafrika zinakosa thamani miongoni mwa wananchi wenyewe. Kwa mujibu wa Kaplan (1989) na Brake (1980), tabia ya ushoga huigwa na kusambazwa kupitia TEHAMA. Njia za TEHAMA kama huduma za mtandao, setilaiti, runinga na redio hutumika kuzalisha tamaduni mpya zinazojikita katika muziki, filamu, mavazi na mitindo ya maisha pamoja na bidhaa wanazotumia. Masuala ya ngono ambayo yalitambulika kama mambo ya faragha na siri, sasa ya wazi (uk. 49).

Utamaduni mpya umeathiri uongozi wa nchi zinazoendelea. Viongozi huiga jinsi nchi zilizoendelea huongozwa na kisha kulazimisha mitindo hiyo ya uongozi katika nchi zao. Alomo (2016) anasema, utamaduni wa nchi zenye nguvu huathiri utamaduni wa nchi zisizo na nguvu na hivyo utamaduni wao hutawala. Katika *Babu Alipofufuka* K anaungana na watu aliowaona kama adui kitambo: mazimwi aliwaita na hata kutangaza vita nao. Lakini leo akiwatazama, anaona kumbe sura zao zinafanana na yake. Anawaona kama watu wazuri na muhimu katika shughuli zake za kisiri. Anatumia watu hawa kuwadhulumu wananchi.

***Utabaka***

Ann (2013) anasema kuwa, utabaka ni hali inayojitokeza katika jamii ambapo watu hujigawa kulingana na mali waliyo nayo, elimu, madaraka kazini ama imani za dini. Kujigawa huko ndiko huibua utabaka. Katika jamii, tuna matabaka mawili, la walionacho na wasionacho na hakuna maelewano kati ya matabaka haya mawili. Kwa upande mwingine, Waafrika wana imani nyingine yenye athari kubwa ya kuwapo kwa ulimwengu wenye matabaka matatu; mbinguni, duniani na chini ya dunia ambako huitwa pia kuzimu. Hii inamaanisha kwamba, mbinguni ndiko anakoishi Mwenyezi Mungu ambaye ndiye muumba wa vitu vyote; duniani wanaishi binadamu walio hai na kuzimu kuna wafu wanaorejelewa na baadhi ya wataalamu kwa jina la wafu hai kama inavyoelezwa na Tempels (1959) na Mbiti (2010). Katika maandiko yake, Mbiti (2011) anafafanua kuwa Waafrika wanaamini kuwa kifo cha mtu ni mabadiliko ya kiumbo kutoka katika mwili halisi aliokuwa nao na kuwa katika umbile la kiroho lisiloonekana.

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, tunaelezwa namna viongozi na matajiri wanavyojilimbikizia mali nyingi huku wananchi wenzao wakibaki katika ufukara. Wanajenga majumba makubwa, kununua na kunyakua mashamba na hata kununua magari mengi. Utajiri wa aina hii unaweka mipaka kati ya matajiri na maskini. Matajiri wanaonesha dhahiri kuwatenga watu wa kawaida, bila wao wenyewe kutambua. Lakini, kama Waswahili wasemavyo, 'Shida haizoeleki,' baadaye wanyonge wanatambua kuwa wamekuwa wakinyonywa na kutengwa na mabwana wakubwa hao. Ndi anasema:

> Mwisho wa yote nilikuja kutambua maana ya vivuli kukimbiana. Hasa vivuli vya watu waliokuwa na nyadhifa kubwa zamani. Wale ambao sasa wameporomoka kama mimi. Hivi vilikuwa vivuli vilivyojitahidi zaidi na zaidi visionekane, isipokuwa vilipokuwa na haja. Wengi wetu tuliokuwa miaka saba iliyopita, tukining'inia hodari katikati pale mabwana wakubwa walipokuja kukata miguu ya ngazi zetu…Ilikuwa kama sisi tunatiwa pumzi za kujichukia. Kila tulipozidi kuvimbiana kwa unene wa pumzi tupu, ndipo tulipojikataa zaidi. Kama watu tulioamka kutoka ndoto ya jinamizi na kujisahau na hatimaye kujiuliza: sisi nani? Asili yetu ipi? Tunatoka wapi? Tupo na tunaelekea wapi? (uk. 29).

Kupitia kwa dondoo hilo, mwandishi anatumia vivuli kumaanisha ishara au mifano ya watu. Watu ambao sasa hawaonekani kama watu kwa sababu ya umasikini wao. Ni watu ambao hapo awali walikuwa tajika hadi walipofutwa kazi na wakubwa wao. Ndi anasema kuwa alipopata digrii yake, alishika kazi mbalimbali serikalini. Aliwahi kuwa mwalimu wa sekondari na pia alifanya kazi katika ofisi za ngazi mbalimbali. Anasema kuwa baada ya mageuzi, kazi za ngazi za juu zilitengwa kwa

wastahiki fulani na wala hazikutegemea kuwa na elimu, akili au busara (kur. 15-16). Wageni walikuwa miongoni mwa watu bora kabisa katika jamii hata kuliko wenyeji. Ndi anapotembea kuelekea barazani, alipita mtaa uliozuka ghafla. Palikuwa pahali chafu na dhaifu, penye vibanda vilivyochipuka ovyo. Vibanda viliyojengwa kwa kitu chochote, kisichofaa-kinachofaa: magongo, fito, papi, matambara, mibacha, majamvi mabovu, maboksi, mapande ya mabati yenye kutu… (uk. 31). Mwandishi anawaonesha kama watu ambao uwepo wao hauna faida yoyote. Japo utengano kama huo ni wazi, mnyonge hawezi kukandamizwa milele kama Kamunde (1983) anavyodhihirisha.

Katika *Babu Alipofufuka*, kuna matabaka ya walio nacho na wasiokuwa nacho yanayoweka mipaka ya kiulimwengu kati ya mtu na mtu. K anatumiwa kama kielelezo cha watu walio katika tabaka la juu, ambao wengi wao ni viongozi wapenda rushwa, wafisadi na wanyonyaji. Wanao- fuja mali ya umma pasipo kujali maslahi ya wanyonge. Mohamed anatueleza aina ya gari analotumia K jinsi lilivyo la nguvu.

Limonsin lilipishana na nyengine zilizokujia upande linakotoka na kushindana kuoneshana makarama ya nguvu. Limonsin ni ishara ya nguvu ndani ya nguvu. Kila siku K alisema. …Upepo ulioingia ndani ya limonsin ulichujwa (kur. 24-25).

Mwandishi anatuonesha thamani ya mali ya K kupitia kwa gari analotumia. Halikuwa gari la kutumiwa na watu wa kawaida. Lilikuwa na chombo fulani cha kisasa ambacho kila baada ya kukibonyeza, kufumba na kufumbua, mapikipiki yaliyokuwa yakiruka angani yalifika na limonsin nalo likaruka likiongozwa na kulindwa na mapikipiki hayo ya polisi nyuma mbele na ubavuni. Aidha, kasri alimoishi K lilikuwa kubwa kiasi cha kufananishwa na kasri la Dracula kwa mujibu wa marafiki zake Delpiero, Von Heim, Di Livio na Miyazawa. Mwandishi anasema:

> Bawa moja la kasri lilipiga hatua kushoto na kupaa angani. …Kila bawa linajitosheleza kwa maskani kamili na meko yake, na kumbi zake, …Mavyumba yake yasiyo idadi yanayojitahidi kwenda juu kama vile jumba la makomanzi. (uk. 15)

Jumba la aina hii halijengwi na mtu yeyote bali watu tajiri. Ni ishara ya tabaka la walionacho. K anajenga jumba kubwa kiasi hicho ilhali wananchi wengine hawana makao.

Bi Muse katika umazingaombwe anamtembeza Ndi katika bustani ya uhalisia na kumwonesha jinsi ambavyo kuna tofauti kubwa kati ya wale ambao wamekumbatia mabadiliko na waliokataa. Bi Muse anasema:

> Tazama! unaona wingi wa vibanda vya ukorofi vile vilivyojiinamia kwa fedheha, kule ambako wivu na uchungu ulianza na kuendelea enzi na azali? Na tazama kule mbali zaidi mijini kunakozidi kupandikizwa minara ya Babeli yenye majina ya kigeni. Kitu gani chenu katika dunia hii? (uk. 65).

Mwandishi anatuonesha jinsi ambavyo mataifa yanayokubali mifumo ya wabeberu yanavyopokea misaada inayowawezesha kuendelea vyema ilhali yale ambayo yamekataa kwenda kulingana na mahitaji yao yanavyosalia nyuma. Kwa mujibu wa Ruigrok na Tulder (1995), Jauch (2001) na Offiong (2001), utandawazi utaboresha maisha ya watu wote duniani. Pia, wanatambua utandawazi kama ngazi ya biashara baina ya nchi, masoko huru ya bidhaa, na kutangamanisha tamaduni mbalimbali. Muse anamwonesha Ndi majumba ya kifahari ambayo yamejengwa kutokana na teknolojia mpya. Anasema kuwa watu hao walioyakumbatia mabadiliko, wana mishahara mizuri hivyo wanaishi maisha mazuri. Upande mwingine anamwonesha mataifa yaliyoipinga teknolojia mpya jinsi yalivyo na wivu na machungu. Mwandishi kupitia mhusika K katika *Babu Alipofufuka*, anatuonesha jinsi ambavyo jengo la Neo-casino ni la kifahari. Kwamba lilijengwa na wageni:

> …inasemekana jinamizi hili limesafiri kutoka mbali kuja kuota hapa kuwafariji watamaduni wapya tu kwa kile wanachokiita fahari. Vinginevyo ungemfaa nani kutoka hali ya kuramba mikono mitupu? (uk. 28)

Mohamed anasema kuwa ukilitazama jinamizi hilo, utaliona linajitangazia ufalme katika mazingira hayo na kwamba fahari yake inakamilishwa ndani si nje. Vyumba vyake vimekogeshwa anga la

umeme na nje limevishwa mikufu ya mataa ya rangi (uk. 29). Maelezo hayo yanadhihirisha kiwango cha umaskini waliomo wananchi kiasi kwamba hawawezi kujenga jengo kama Neo-casino na hata baada ya wageni kulijenga, linawafaa wachache tu, matajiri na viongozi.

Kupitia kwa mlolongo wa magari ambamo K anapatikana akielekea Neo-casino, mwandishi anatuonesha kiwango cha umaskini ambacho kinatawala maeneo yale. Anasema:

> Watoto viditia na vitumbo vyao na nguo zilizowazidi vimo kuifanya miili yao mifupa mitupu ipwae zaidi… Wakubwa wamewabeba wadogo na wengine vijana, hirimu, makamu, wazee…wote walikuwa wakikaribia. Watoto walikuwa wakigonga vioo na kunyoosha mikono kuomba pesa. Vijana walikuwa wameghadhabika na kufinyanga ngumi ambazo kila baada ya muda ziliishia kupiga bodi la limonsin (kur. 26-27).

Tabia hiyo ya wananchi kuikaribia limonsin ili kuomba msaada inaonesha kiwango cha umaskini walimo ndani. Watoto kuomba pesa na kuigonga limonsin ni ishara ya ghadhabu walizo nazo. Pia, kuna wale ambao walikuwa wamejaa mori na macho yao yaliwaka moto wa kisasi. Wao walijaribu kuliinua gari ili kulipindua. Marx (1973) anafafanua kwamba, matabaka huwa katika hali ya mikinzano na kwa sababu jamii daima ziko katika harakati za kufanya maslahi yao bora, mikinzano hii huleta mapinduzi na uongozi kuchukuliwa na tabaka la wafanyakazi na mafalahi. Mivutano ya kijamii huchangia kuyaleta mabadiliko yanayohitajika katika jitihada za jamii za kilimwengu kuacha hali zao dhaifu na kuukaribia utu kamili. Kwa hiyo katika kujaribu kulipindua limonsin, mwandishi anatuonesha nguvu walizo nazo wananchi za kuweza kujikwamua kutokana na unyanyasaji wa matajiri na viongozi wabinafsi.

Kama anavyo sema Kenan (1983), umaskini hudhihirika katika kazi za fasihi kupitia usawiri wa wahusika kimatendo, kiusemi, kimazingira na kwa muonekano wa nje, Mohamed anaonesha jinsi ambavyo jinamizi hilo la umaskini linavyowafinyilia na kuwaumiza wananchi huku viongozi wakijilimbikizia mali kupita kiasi. Katika riwaya ya *Dunia Yao*, ukosefu wa fedha ndio chanzo cha Ndi kupatwa na wazimu wa kunyamaza. Hawezi akaijukumia familia yake baada ya kupoteza ajira yake. Ni kutokana na hali hii ndipo tunamwona Yungi akijiingiza katika kazi ya ukahaba ili aweze kuiokoa familia yake (kur. 23-27).

Akielekea barazani, Ndi anakutana na kijana mmoja ambaye anamdanganya kuwa aliharibikiwa na kibofu cha mkojo na kwamba alifanyiwa operesheni na kutiwa kipira ambacho sasa kimepasuka hivyo anahitaji msaada ili anunue kingine. Ndi anagundua ujanja wake (uk. 155). Mohamed anatumia maelezo haya kutuonesha kiwango cha umaskini, kiasi cha kuwafanya watu kusingizia ugonjwa ambao hawana mradi wapate msaada. Hili si jambo la kawaida kulingana na maadili ya Kiafrika, lakini wakati mwingine inawabidi watu kudanganya ili waweze kuishi.

Mwandishi katika *Babu Alipofufuka* anasema, Mungu tu ndiye ajuaye vipi huvinusuru viumbe vyake, vipi wokovu wa kutia na kutoa mkono kinywani huja ni miujiza mitupu! Tunaoneshwa jinsi ambavyo kupata chakula ni bahati tu kwa watu hawa. Katika kiini cha jiji, taa za umeme hafifu zikifanya kazi ya bure kulimeza giza ilhali kule kwenye tambarare la mitaa ya Madongoporomoka giza lilitangaza ushindi (uk. 30). Mwandishi anatueleza kiwango cha umaskini uliokithiri maeneo mengine ilhali kwingine utajiri wa hali ya juu umedhihirika. Kupitia kwa Mzuka, mwandishi anatuonesha kiasi cha utengano baina ya K na wananchi. Mzuka anamweleza:

> … ndani ya nyoyo zenu mnalazimisha kuwepo utengano mkubwa namna hiyo… Nia ni kujisikia kuliko jambo jingine lolote. Na kwa sababu hiyo ndiyo maana umeihisi safari ndefu. Ukweli wa mambo ni kuwa pamoja na kutengana nao kwa makasri, mabustani, magari na starehe kemkem, mmepakana na dunia yao inayonuka. Harufu mnazisikia lakini mnaziba pua… (uk. 88).

Dondoo hilo linakashifu tabia ya viongozi ya kulazimisha kuwepo kwa matabaka katika jamii. Mwandishi anamwambia K kuwa hata kama wanalazimisha utengano wa aina ile, athari zake hawaziepuki kamwe. Kutokuishi vizuri kwa watu wa tabaka la chini lazima kuwaathiri watu wa

tabaka la juu. Hii ni kwa sababu Mohamed anasema wamepakana tu, wanaishi karibu. Maskini wanapokosa mahitaji yao ya kimsingi, inabidi wajiingize katika matendo maovu kama vile wizi. Hii inamaanisha kuwa maisha ya matajiri huwa hatarini, hawako

salama pamoja na mali yao.

***Uongozi Mbaya***

Uongozi ni madaraka anayopewa mtu kusimamia shughuli au asasi (TUKI, 2004). Pia, ni mojawapo wa taasisi za mahusiano. Uongozi mbaya ni aina ya utawala ambapo kiongozi hafuati sheria katika kutekeleza majukumu yake. Ubinafsi na ufisadi ni tabia walizonazo baadhi ya viongozi ambao matendo yao huwa ya kujinufaisha tu pasi na kuwajali wenzao. Althusser (1981) anasema kuwa, sheria hutumiwa kuendeleza itikadi ya kitawala wala si kulinda haki. Aidha, mifumo ya kitawala kama demokrasia ni asasi mojawapo ya kunyamaz isha watu badala ya kutumiwa kwa maslahi yao.

Katika riwaya ya *Dunia Yao*, mwandishi anatueleza namna viongozi walioshika hatamu wanavyokosa kuwajali wananchi. Kutokana na hali hii, viongozi wengi wa bara la Afrika wamekuwa 'Miungu-watu'. Wamechukua kila kitu kutokana na ubinafsi wao. Aidha, kutokana na ubaya wao, wamekuwa wakikiuka haki za kibinadamu na matokeo yake ni kutawala kimabavu. Viongozi hawa hufanya uamuzi wa mambo mengi na kulazimisha kutekelezwa kama wanavyotaka. Mhusika Mimi (Ndi) anasema:

> Najua mimi…najua kwa nini hutaki kubadilika mtu wewe? Hata wahakiki wako wanakusema…Naam, kama unavyojua. …Wamechukua kila kitu! Wao wamekuwa ndio wafikiri wetu. Wasemaji wetu. …Walimu, madaktari, wanafalsafa, wanauchumi, mashehe, mapadri na walinzi wetu. Kwa jumla waendesha maisha yetu yote. Sehemu za viwiliwili na akili zetu. Kwa ufupi wao ni kila kitu chetu! (uk. 43).

Kutokana na hali inayoelezwa katika dondoo hili, kuna baadhi ya watu ambao huamini kwamba, bado uhuru wa bara la Afrika haujazaa matunda. Hii inatokana na viongozi wetu kuvaa majoho ya kikoloni na kuendeleza ukandamizaji wa tabaka la chini. Ni kwa sababu ya utawala mbaya ambapo Ndi na wahusika wengine waliokuwa na nyadhifa serikalini wanajaribu kufanya mapinduzi. Jaribio ambalo linawapelekea kupoteza kazi zao na kuishi katika upweke. Baadaye, polisi wanamkamata Ndi na kumpeleka jela. Mwandishi kupitia kwa mhusika Ndi anaonesha utawala mbaya wa kunyimwa haki ya kujieleza kwa wanajamii.

K katika *Babu Alipofufuka* ametumiwa kuonesha ujeuri walionao baadhi ya viongozi kwa sababu ya mali zao. Anaonekana kutowajali wananchi anaowaongoza. Mohamed anasema:

> …jeuri kwa hakika inakuja kutokana na umoja wao na kwa namna hiyo jeuri ni yake pia. Hajali kabisa, hajali hata kama angeumbwa peke yake duniani maadamu dunia ingempa ladha tamu namna hiyo. Wanaozama na wazame, wanaodidimia wadidimie mtu husimama kwa miguu yake (uk. 17).

K ni mfano wa viongozi wanaoyajali maslahi yao wenyewe. Msimulizi anasema kuwa kanuni hiyo ya utamaduni mpya inapatana fika na tabia yake. K anasema kuwa wakakamavu pekee ndio wana haki ya kupanda juu ya mabega ya watu wengine na kukalia vichwa vyao (uk. 101). Anamaanisha kuwa wao ndio wanaweza kuwatawala wananchi na kujinyakulia mali wapendavyo. Wakati K anapata barua kutoka kampuni ya Kijerumani aliyotiliana nayo saini kuanzishwa FKK ikimwarifu kuwa shughuli za ujenzi wa kijiji kizima inatazamiwa kuanza mara moja, hivyo afanye haraka kutafuta pahala panapofaa, shuruti za pahala panapofaa zilianzishwa (uk 75). K anatumia mamlaka aliyonayo vibaya kwa kuwashurutisha watu kuhama kwenye mashamba yao ili apate nafasi ya kujenga mradi wake.

Katika umazingaombwe, kwenye mazungumzo baina ya kiongozi wa wakati na K pale mbele ya mahakimu, K anasomewa mashtaka yake. Kupitia kwa mashtaka haya, mwandishi anatujulisha baadhi ya mambo aliyoyafanya. Anasema:

> Umeshtakiwa na roho nyingi ulizozikatisha tamaa au hata kuziangamiza kabisakabisa kwa ulaghai na uhasidi wako…wamekushtaki pia kwa hatia ya uwambangoma … na kwa kushiriki kuwageuza watu wote panya wa majaribio… majaribio ambayo yamevunja na kuharibu maisha yao yote… (uk 143).

Maelezo haya yanaonesha uovu na ukatili walionao wengi wa viongozi wa bara la Afrika. K ni mfano wa viongozi wanaowanyang'anya wananchi mali yao kwa nguvu na iwapo wazungu wanawahitaji watu wa kutumiwa kufanya majaribio ya kisayansi, wanawatoa wananchi wao. Hili ni tendo linalokashifiwa mno na Mohamed.

***Sanaa Mpya***

Sanaa mpya inarejelea fasihi mpya isiyo na namna moja ya utunzi (Kandagor, Ongechi na Vierke, 2017). Fasihi ya Kiswahili imepitia mikondo miwili mikuu tangu kuchipuka kwake. Katika mkondo wa kwanza, kazi za fasihi zilikuwa za kihalisia zilizofuata misingi jadi ya uandishi pasipo ukiushi wa lugha na matukio yanayojitokeza ndani yake na mkondo wa pili wa uandishi wa kazi za fasihi ambao ni wa kimajaribio. Mulokozi (1996) na Senkoro (2006) wanasema, lengo kuu la kuzuka kwa mkondo huu lilikuwa ni kufufua fasihi ya Waafrika ambayo ilionekana kumezwa na kaida za uandishi za Kimagharibi.

Katika *Dunia Yao*, Bi Muse anayehusishwa na ghamidha na kariha ya utoaji wa sanaa za kiubunifu huko Ugiriki, ni mshirika wa kiroho wa mhusika jumui Ndi. Bi Muse anazua mjadala mpevu wa swala zima la sanaa na hulka yake kama inavyowasilishwa na Mohamed. Anaeleza namna anavyoweza kubadili umbo na kuwa mwenza wa kila msanii duniani. Ingawa amezaliwa na Mungu mkuu wa Ugiriki, Zeus, Bi Muse ana uwezo wa kuwa binti wa kifalme au wa kijini kwa kuzingatia utamaduni wa msanii husika. Ni mungu wa Waswahili na ana nguvu za kichawi za kumzuga mtu na kummiliki pale anapomchagua na kumfanya kuwa kiti chake.

Mohamed anasema kuwa uandishi hufuatwa na ghamidha na kariha inayomjia mwandishi na wala si jambo la vivi hivi tu, chambilecho Ndi kuwa Muse si kiumbe wa 'sasambura turore' au anayejitoa hadharani kuonekana. Mwandishi anaufafanua uhusiano wa Ndi na Muse kama wa mke na mume wanaoliwazana na kubembelezana hadi wanapooana na kuwekana nyumbani. Ni taswira ya unganiko la kipekee ambalo hufukuza utasa na badala yake huzalisha kazi za kisanaa baada ya wahusika hawa kusuhubiana na hata kupata mtoto, yaani kazi inayotungwa. Ndi anaeleza hatua hizi hivi:

> …si kiumbe wa sasambura turore. Hujifichua anapohitajiwa kwa mapenzi ya dhati au kwa kutoa msaada. Na mimi, nimefikia baleghe ya kusalitika naye. Nina haja naye …Anisaidie kuukata ugumba wa utunzi. Nina hamu kurutubisha na kutia mbolea pahala fulani. Nipate kizazi kipya cha sanaa katika ukame wa ubunifu. Nipate kurutubisha kizazi kipya cha utu katika ukame usio na utu (uk 61).

Mwandishi anamtumia Muse kuwajulisha wasanii kuwa wakati wa uandishi wa kazi za kiuhalisia umepita. Anamwambia Ndi kuwa amekuja kumnusuru asiangamie katika usanii, kumwinua katika raha na madadi ya mwinuko wa kisanaa (uk. 69). Mohamed anaeleza umuhimu wa kukumbatia usanii mpya ili wasanii wasipotoke kwa kupitwa na wakati.

Mwansishi anatueleza kupitia kwa Ndi kuwa awali wasanii walikumbwa na changamoto si haba katika uchapishaji wa kazi zao za kimajaribio lakini sasa zinakubalika. Anasema:

> Kwa kweli wakati ule nilipoanza, nisingeweza kuandika vingine nje ya uhalisia. Kanuni zake zisingekubali. Nani angechapisha? Nani angenisoma? (uk. 71).

Fasihi mpya ilionekana kuwa changamani na isiyoeleweka moja kwa moja. Jambo ambalo lilifanya uchapishaji wake kuwa mgumu. Wachapishaji waliona kuwa hakuna mtu angenunua vitabu vyenye fasihi kama hiyo, hivyo walisusia kuvichapisha. Lakini leo, Mohamed anawahimiza wasanii kuchapisha kazi za kimajaribio kwani zinakubalika na kusomwa na watu wengi.

Ndi, kama wasanii wengine, amekuwa katika hali ya mpito. Uhalisia aliouenzi, hauna nafasi kwake kwa kuwa wasomaji sasa wako tayari kuzipokea kazi za kimajaribio. Awali, hakuwa na budi

ila kutunga kazi za kihalisia kwa sababu anazozieleza katika majadiliano yake na Muse. Jambo la kwanza, wasomaji walikuwa na matarajio au dukuduku lao kuhusu kazi za fasihi ambazo walitarajia ziandikwe kwa mtindo huo wa kihalisia. Pili, wachapishaji hawangethubutu kuchapisha kazi za kimajaribio kwa kuwa wanunuzi hawangeziona za manufaa kwao. Hivyo mwandishi wa wakati huo hangekuwa na hiari ya kiuandishi ila kuwatii wachapishaji ambao waliongozwa zaidi na faida inayotokana na mauzo yao kuliko ujasiri wa kisanii wa mwandishi.

Wataalamu mbalimbali (Khamis 2008; Mwamzandi, 2013) wanakubaliana kuwa uchopekaji wa vipande vya simulizi ni mtindo mamboleo unaokiuka kaida za awali za uandishi wa kimapokeo uliokuwa na muundo wenye muumano na mshikamano. Kama anavyosema Khamis (2003), matumizi ya vipande vidogo vya hadithi visivyounganika vizuri ni mbinu ya kimakusudi anayoitumia mwandishi kama dhihirisho la ukosefu wa mshikamano katika jamii ya kisasa barani Afrika. Riwaya teule kama mojawapo ya riwaya za Kiswahili zilizotumia mbinu ya uchopekaji wa simulizi zimedhihirisha ukweli huu kama inavyojitokeza katika dondoo linalofuata kutoka kwenye riwaya ya *Dunia Yao*:

> Katika simulizi na mapito yake, vipandevipande –si lazima vishikane. Unavimwaga tu vipande vyenyewe kama unaatika mbegu kwenye shamba la sanaa. Unafanya hivyo kuwaacha wasomaji waunge wenyewe vipande vya maana zao, huku maneno mengine ukiyajengea vivuli ili kuwatenga makusudi watafute maana zao badala ya kuzipata maana kibungabunga...kipande hapa... kipande pale. Vipande vya 'allegory'. Vipandevipande vya ngano mpya. Ngano ya tafrani-za-kileo katika usogori mpya (uk. 9; 68).

Katika dondoo hili, tumeelezwa kuwa simulizi katika kazi ya fasihi hujikita katika 'tafrani-za-kileo'. Kwa mujibu wa kamusi ya TUKI (2018) tafrani ni fujo, ghasia au hali ya kutokuwa na utulivu. Kwa hivyo, simulizi za tafrani za kileo ni simulizi zinazozungumzia fujo, ghasia na ukosefu wa mshikamano katika ulimwengu wa sasa. Aidha, tumeelezwa kwenye dondoo kuwa ni jukumu la msomaji kuunga vipandevipande hivyo vya hadithi ili kuwasilisha maana zao mwenyewe. Haya ni kweli katika riwaya tulizoshughulikia katika tasnifu hii kwa sababu maudhui yanayopatikana yamechopekwa huku na huku bila mpangilio maalumu. Ni jukumu la msomaji au mtafiti kuyakusanya na kuyaunganisha pamoja ili yaweze kuelezeka. Uchopekaji wa vipande vya simulizi katika *Dunia Yao* na *Babu Alipofufuka* umejitokeza kupitia matumizi ya visa na vijihadithi vingi visivyokuwa na mshikamano.

Riwaya za kimajaribio, kama inavyopendekezwa, zimejengwa na vipande vya ngano au simulizi fupifupi zisizokuwa na uaushi, tofauti na simulizi kuu ambazo Lyotard (1984) aliziona kama zilizopoteza thabiti zao. Simulizi hizi hutokeza kwa muda mfupi ndani ya riwaya na hazilengi kuhodhi ukweli kama zilivyo simulizi za jadi ambazo zililenga kukongomea ukweli kama zilivyouona. Lyotard amenukuliwa na Barry (2002) akisema kuwa simulizi kuu hubuniwa kwa azma ya kusawazisha ukinzani na kusababisha urajua ambao kwa hakika hauna mashiko. Mtazamo sawa na huu unachukuliwa na riwaya teule kutokana na kile anachokirejelea Baudrillard (1983) kama "kupotea kwa uhalisi" ambapo mpaka kati ya uhalisi na kinachodhaniwa kuwa maana yake haupo.

**Hitimisho**

S. A. Mohamed amefaulu katika kuwatumia wahusika jumui Ndi na K kuwasilisha maudhui mbalimbali katika riwaya teule. Kimaudhui, fasihi ya kimajaribio ina mtazamo wa kuyaona matatizo ya jamii kwa msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu ya matatizo yote yanayoikumba jamii. Katika riwaya ya *Dunia Yao* mwandishi amemtumia Ndi kuibua maudhui tofauti katika uhalisia na katika umazingaombwe akiwa Ye na Shaib kudhihirisha ujumui wake. Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, amemtumia K katika uhalisia na pia katika umazingaombwe akizumgumza na Mzuka na wafu kuibua maudhui tofautitofauti yaliyoangaziwa.

**Marejeleo**

Alomo, O. S. (2016). *Uwakilishaji wa Utandawazi katika Riwaya Mpya ya Kiswahili Iliyoandikwa na S. A. Mohammed na K. W. Wamitila* (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Egerton.

Althusser, L. (1968). *Reading Capital*. Paris: Librairie Francois Maspero.

Barry, P. (2002). *Beginning Theory*. Manchester: Manchester University Press.

Baudrillard, J. (1983). *Simulations*. New York: Semiotext(e).

Bergonzi, B. (1972). *The Situation of the Novel*. London: Penguin Publishers.

Brake, M. (1980). *The Society of Youth Culture and Youth Subcultures: Sex, Drugs and Rock 'n' Roll?* London: Routledge and Kegan Paul.

Friedman, T. L. (2005). *The World is Flat: A Brief History of the Twenty-First Century*. New York: Farrar Straus and Giroux.

Gromov, M. D. (1998). Nagona and Mzingile Novels, Tale or Parable? *Swahili Forum, 5*(55), 73-78.

Jerono, P. (2016). Taaluma ya Uanahabari na Kiswahili katika Enzi ya Utandawazi. L. C. Mwita. (Mh.). *Kiswahili na Utandawazi*. Nairobi: Twaeza Communications, 105-115.

Kamunde, M. (1983). *Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed.* (Tasnifu ya Uzamili) (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kamusi ya Karne ya 21 (2011). (Toleo la Pili). Nairobi: Longhorn Publishers.

Kenan, R. S. (1983). *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge.

Khamis, S. A. M. (2017). Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili. *Kioo cha Lugha, 5*(1), 13-23.

Lee, G. (2004). *A Million Little Choices: The ABCs of CNF*. London: Yale University Press.

Marx, K. (1973). *On Literature and Art*. New York: International General.

Mbiti, J. S. (2010). *Introduction to African Religion*. Kampala: East African Educational Publishers, Ltd.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religion and Philosophy*. Kampala: East African Educational Publishers Ltd.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Mohamed, S. A. (2006). *Dunia Yao*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Ltd.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mwamzandi, I. Y. (2013). Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia ya Fasihi. *Swahili Forum*, *20*, 48-66.

Roh, F. (1925). *Magic Realism: Post–Expressionism. Magical Realism, Theory, History, Community*. Durham: Duke University Press.

Selfe, P. (1993). *Alevel Sociology: Trends and Patterns* (2nd Ed.). London: Macmillan Press Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (2007). Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe. *Kioo cha Lugha*, *5*, 1-12.

Tempels, P. (1959). *Bantu Philosophy*. Paris: Presence Africaine.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu). Dar es Salaam: Oxford University Press.

Walibora K. (2010). Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*. *Swahili Forum*. 17 kur. 143-157.